

KUMFAHAMU MWENYEEZI MUNGU NDANI YA QUR'ANI

<"xml encoding="UTF-8?">

BISMILAHİ RAHMANİ RAHIYMI

KUMFAHAMU MWENYEEZI MUNGU NDANI YA QUR'ANI

NJIA ZA KUMFAHAMU MWENYEENZI MUNGU 2

katika makala iliyopita (makala namba moja) tulielezea nyenzo zinazomuongoza mwanaadamu katika kumfahmu Mwenyeezi mungu. katika sehemu hii ya pili tutaendelea .kuzielezea nyenzo hizo na kuzithibitisha kwa aya za qur_ani

.DALILI ZA KIAKILI

?Hivi kweli kiarabu hiki cha Qur-ani yuko binaadamu anayeweza kukiandika au kukisema

Ndani ya kitabu kitukufu cha Mwenyeezi Mungu kuna aya nyingi za Qur-ani kariym zinazomtaka mwanaadamu afikiri kiakili na awe makini . Miongoni mwa aya hizo ni hizi -:zifuatazo

Madhalimu kweli hawa- kama ilivyo katika aya ya 17- wa nafsi zao na kuwadhulumu viumbe wengine wanaowapoteza makusudi. Sio kama wanavyodai baadhi yao, na tunathibitisha hayo -:kutokana na aya hizi zifuatazo

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنْزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ[1]

Na ambao wanayaamini yaliyo teremshwa kwako, na yaliyo teremshwa kabla yako; na Akhera .wana yakini nayo

وَلِلَّهِ الْمَشْرِقُ وَالْمَغْرِبُ فَأَيْنَمَا تُوَلُّوا فَثَمَّ وَجْهَ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ وَاسِعٌ عَلِيمٌ[2]

Na mashariki na magharibi ni za Mwenyezi Mungu. Basi kokote mnako elekea, huko Mwenyezi .Mungu yupo. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa na Mjuzi

صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ[3]

.7. Njia ya ulio waneemesha, siyo ya walio kasirikiwa, wala walio potea

يَا قَوْمِ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِنْ أَجَرِيَ إِلَّا عَلَيَّ الَّذِي فَطَرَنِي أَفَلَا تَعْقِلُونَ[4]

Enyi watu wangu! Sikuombeni ujira kwa ajili ya haya. Haukuwa ujira wangu ila kwa Yule aliye
?niumba. Basi hamtumii akili

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رَجَالًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ
مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا أَفَلَا تَعْقِلُونَ[5]

Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipo kuwa wanaume tulio wafunulia wahyi miongoni
mwa watu wa mijini. Je! Hawatembei katika ardhi wakaona jinsi ulivyo kuwa mwisho wa walio
kuwa kabla yao? Na hakika nyumba ya Akhera ni bora kwa wamchao Mungu. Basi
?hamfahamu

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ أَفَلَا تَعْقِلُونَ[6]

Na hakika tumekuteremshieni Kitabu ambacho ndani yake yamo makumbusho yenu. Je!
?Hamzingatii

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَعِبٌ وَلَهُمْ وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ[7]

Na maisha ya dunia si chochote ila ni mchezo na pumbao tu. Na hakika nyumba ya Akhera ni
?bora zaidi kwa wanao mcha Mungu. Basi, je, hamtii akilini

اتَّامِرُونَ النَّاسَ بِالْبِرِّ وَتَنْسَوْنَ أَنْفُسَكُمْ وَأَنْتُمْ تَتْلُونَ الْكِتَابَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ[8]

Je! Mnawaamrisha watu mema na mnajisahau nafsi zenu, na hali nyinyi mnasoma Kitabu?
?Basi je, hamzingatii

Maelezo kuhusiana na aya

Baadhi ya wanavyuoni wa Kiyahudi wakisilimu jamaa zao wakapata habari, huwaendea kwa siri
wakawaambia “ Dini hii mliyoifuata aliyokuja nayo nabii Muhammad ni haki, shikamaneni nayo;
lakini sisi hatuwezi kukosa ukubwa wetu” ndiyo Mwenyeenzi Mungu anawasimanga kwa aya
.hii

إِنَّا جَعَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ[9]

.Hakika Sisi tumeifanya Qur'ani kwa Kiarabu ili mfahamu

قَالَ رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَا إِنْ كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ[10]

Musa) akasema: Ndiye Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi na viliomo baina yao, ikiwa)
.nyinyi mnatia akilini

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لِمَ تُحَاجُّونَ فِي إِبْرَاهِيمَ وَمَا أُنْزِلَتِ التَّوْرَةُ وَالْإِنْجِيلُ إِلَّا مِنْ بَعْدِهِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ [11]

Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahim, na hali Taurati na Injili
?hazikuteremshwa ila baada yake? Basi hamzingatii

اعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا قَدْ بَيَّنَّا لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ [12]

Jueni kwamba Mwenyezi Mungu huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Tumekubainishieni
.Ishara ili mpate kuzingatia

فَقُلْنَا اضْرِبُوهُ بِبَعْضِهَا كَذَلِكَ يُحْيِي اللَّهُ الْمَوْتَى وَيُرِيكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ [13]

Tukasema: Mpigeni kwa kipande chake (huyo ng'ombe). Ndivyo hivi Mwenyezi Mungu
.huwahuisha wafu; na anakuonyesheni Ishara zake ili mpate kufahamu

كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ [14]

وَإِذَا لَفُؤَ الَّذِينَ آمَنُوا قَالُوا آمَنَّا وَإِذَا خَلَا بِغُسْهُمْ إِلَى بَعْضٍ قَالُوا أُنْحَدُّثُوهُمْ بِمَا فَتَحَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ لِيُحَاجُّوكُمْ بِهِ عِنْدَ
رَبِّكُمْ أَفَلَا تَعْقِلُونَ [15]

Na wanapo kutana na wale walio amini husema: Tumeamini. Na wanapo kuwa peke yao, wao
kwa wao, husema: Mnawaambia aliyo kufunulieni Mwenyezi Mungu ili wapate kukuhojieni
. mbele ya Mola wenu Mlezi? Basi hamfahamu nyinyi

Maelezo kuhusiana na aya

Mayahudi walipokuwa wakimnafikia Mtume (s.a.w.w) na wafuasi wake na wakiwakubalia kuwa
kweli Mtume Muhammad (s.a.w.w) katajwa katika Tawrati, wenzao walikuwa wakiwalaumu
kwa kule kuwafunulia Waislamu mambo ambayo mayahudi wamewafikiana kuwa wayafiche.
Basi Mwenyeenzi Mungu Anawajibu kwa aya ifuatayo, kwamba Yeye anayajua wanayoyaficha
.na wanayoyadhihirisha

SuratI_baqara aya ya 4 [1]

Suratul-baqara aya ya 115 [2]

Suratul-Faatiha aya ya 7 [3]

Surat Hud aya ya 51 [4]

Surat Yussuf aya ya 109 [5]

Surat Anbiyaa aya ya 10 [6]

Surat Al-an-am Aya ya 32 [7]

Suratul-Baqar aya ya 44 [8]

Surat Azukhruf aya ya 3 [9]

Surat ashuaraa aya ya 28 [10]

Surat Al-imrani aya ya 3 [11]

Surat alhadiyd aya ya 17 [12]

Surat Albaqara aya ya 73 [13]

Surat Albaqara aya 242 [14]

Surat Albaqara aya ya 76 [15]

MWISHO